



**SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR  
MAHAKAMA KUU**

EMAIL: [registrar@judiciaryzanzibar.go.tz](mailto:registrar@judiciaryzanzibar.go.tz)

KUMB: MMK/BE/04.G/VOL II

AFISI YA MRAJIS  
S.L.P 160,  
VUGA,  
ZANZIBAR.

TAREHE: 29 JANUARI, 2018.

**TANGAZO**

**MRAJIS WA MAHKAMA KUU ANAWATANGAZIA WANANCHI WOTE KUHUDHURIA KATIKA SHEREHE ZA KUADHIMISHA SIKU YA SHERIA ZANZIBAR KWA MWAKA 2018 RATIBA YA SHEREHE HIZO ITAKUWA KAMA IFUATAVYO**

**TAREHE SITA FEBUARI JENGO LA MAHAKAMA YA WILAYA MWANAKWEREKWE LITAFUNGULIWA RASMI WAKATI TAREHE SABA ASUBUHI JAJI MKUU ATATUNUKU VYETI KWA MAWAKILI HAPO KATIKA UKUMBI WA BARAZA LA WAWAKILISHI LA ZAMANI KIKWAJUNI.**

**TAREHE TISA HAPO KATIKA VIWANJA VYA MAISARA MAONYESHO YA SIKU YA SHERIA YATAFUNGULIWA WAKATI WA ALASIRI.**

**TAREHE KUMI JAJI MKUU ATAONGOZA MATEMBEZI KUTOKA MAHAKAMA KUU VUGA HADI VIWANJA VYA MAISARA SAA 12 ASUBUHI.**

**KWA PEMBA MATEMBEZI KAMA HAYO YATAANZIA MAHAKAMA KUU CHAKE CHAKE HADI KIWANJA CHA MICHEZO GOMBANI SAA 12 ASUBUHI.**

**KILELE CHA SIKU YA SHERIA ZANZIBAR NI TAREHE 12 FEBRUARY KATIKA UKUMBI WA BARAZA LA WAWAKILISHI LA ZAMANI.**

**NA JAJI MKUU OMAR OTHMAN MAKUNGU ATAKAGUA GWARIDE RASMI NA KUASHIRIA UFUNGUZI WA MAHAKAMA KWA MWAKA HUU.**

**KAULI MBIU YA MWAKA HUU NI  
“IMARISHA UTAWALA WA SHERIA KATIKA KUKUZA  
UCHUMI WA NCHI”**

**AHSANTENI NYOTE MNAKARIBISHWA.....!**

